



SAUTI YA DLDM

Toleo Na. 1: Aprili - Juni 2014

ISSN: 123-452



Jukwaa la Wadau

Ndani ya Toleo hili

- Baraza la Famasi lapata msajili mpya
- Karibu Sauti ya DLDM
- Tahariri
- Vyama vya DLDM vyashika kasi
- Halmashauri ya Jiji la Arusha yakabiliana na uhaba wa watoa dawa wa DLDM
- PSI-Tanzania yashirikiana na Baraza la Famasi kubadili muonekano wa maduka ya dawa muhimu
- Watoa dawa wa DLDM 358 mkoani Rukwa wapata mafunzo ya rejea
- Matumizi ya teknolojia yapewa kipaumbele katika usimamizi wa mpango wa DLDM
- Kundi la kwanza la wanafunzi wa kozi ya mwaka mmoja ya utoaji dawa wafanya mitihani ya kuetimu
- Maswali na Majibu: Msajili wa Baraza la Famasi azungumzia dira ya mpango wa DLDM



Imetolewa na:

Baraza la Famasi Tanzania
S. L. P. 31818 Dar es Salaam
Simu: +255 22 245 1007
Tovuti: www.pharmacycouncil.go.tz

Imeandaliwa na:

Medianet Limited
S. L. P. 8608 Dar es Salaam
Simu: +255 22 270 288
Barua-pepe: info@medianettz.com

Imedhaminiwa na:

Shirika la Management Sciences
for Health (MSH) kupitia mradi wa
kuendeleza upatikanaji wa dawa
katika sekta binafsi (SDSI project).



Bi. Elizabeth Shekalaghe

Mnamo Aprili 2014, Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii, Dr. Seif Rashid alimteua Bi. Elizabeth Shekalaghe kuwa Msajili wa Baraza la Famasi Tanzania, akichukua nafasi hiyo kutoka kwa Bi. Mildred Kinyawa aliyestaafu mnamo Desemba 2013 baada ya kulitumikia baraza hilo kwa miaka kumi.

Bi. Shekalaghe anachukua uongozi wa baraza wakati mamlaka na shughuli za baraza zimeongzwa kwa kiasi kikubwa sana kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Famasi ya mwaka 2011. Sheria hiyo inalipatia baraza mamlaka ya kusimamia huduma zote za kifamasia nchini na hii inajumuisha usimamizi mzima wa mpango wa Duka La Dawa Muhimu (DLDM) ambao hapo awali ulikuwa chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Chakula na Dawa nchini Tanzania (TFDA).

Uteuzi huo umepokelewa kwa shauku kubwa na wadau mbalimbali katika sekta ya famasi nchini ambao sasa wanamtegemea Bi. Shekalaghe kuleta mabadiliko katika uongozi wa baraza yatakayoliwezesha kwenda sambamba na majukumu na mamlaka zaidi yatokanayo na Sheria ya Famasi ya mwaka 2011. Bi. Shekalaghe anategemewa kutumia uzoefu alioupata akiwa mratibu wa kitaifa wa mpango wa DLDM chini ya TFDA, na nafasi yake kama rais wa Chama cha Wafamasia Tanzania kuleta tija katika nafasi yake kama msajili wa Baraza la Famasi.

Karibu Sauti ya DLDM

Utekezaji wa mpango wa Duka la Dawa Muhimu umetoka mbali. Mchakato ulianza mnamo mwaka 2001 na tathmini ya sekta ya famasi nchini iliyofanywa na Bodi ya Famasi kwa ushirikiano na shirika lisilo la kiserekali la MSH (Management Sciences for Health) kupitia mkakati wake wa kuongeza upatikanaji wa dawa (SEAM programme). Tathmini hiyo ilionyesha mapungufu mengi katika uendeshwaji wa maduka ya dawa baridi ambayo kipindi hicho yalikuwa yanachangia karibu asilimia themanini (80%) ya huduma za dawa na bidhaa za afya katika sekta binafsi.

Tathmini hiyo iliyafungulia njia majaribio ya mpango wa DLDM katika mkoa wa Ruvuma kati ya miaka 2003 na 2004, upanuzi wa utekezaji katika mikoa ya awali (Mtwara, Rukwa na Morogoro) kwa usimamizi wa ngazi ya taifa, na upanuzi wa haraka sana wa kitaifa kupitia halmashauri za wilaya kuanzia mwaka 2009. Kufikia Machi 2014, maduka ya dawa muhimu 5,757 yalikuwisha sajiliwa katika maeneo mbalimbali ya Tanzania Bara na mamlaka husika (TFDA na Baraza la Famasi) na watoa dawa 18,980 kupewa mafunzo malaam ya DLDM. Lengo kuu la mpango huu ni kuongeza upatikanaji wa dawa zenye ubora uliodhibitishwa na huduma za kifamasi vijijini na pembezoni mwa miji ambapo upatikanaji wa huduma za famasi ni adimu au hazipo kabisa.

Pamoja na majaribio yenye mafanikio makubwa, upanuzi wa kimkoa wenye tija na utekezaji wa haraka wa kitaifa, mpango wa DLDM haujawahi kuwa na chombo maalum cha kuelezea taarifa za utekezaji ikiwemo mafanikio, mafunzo, njia bora za utekezaji na hata changamoto. Habari nyingi kutoka kipindi cha majaribio mpaka utekezaji wa kitaifa zimekosa usimulizi wa kutosha kutokana na ukosefu wa chombo maalum cha habari kilichotengwa kwa ajili ya mpango huu.

Sauti ya DLDM linadhamiria kuziba pengo hili kwa kuwapa wadau wote sauti katika kuelezea maendeleo ya mpango wa DLDM. Malengo mengine ni kuwajulisha na kuwaelimisha wadau juu ya shughuli mbalimbali za mpango; kutoa njia ya mawasiliano baina ya mamlaka husika na watekezaji wakuu wa mpango katika ngazi ya wilaya na jamii; na kutumika kama chombo maalum cha kuongezea hadhi mpango wa DLDM katika ngazi za taifa na kimataifa.



Mtoa dawa wilayani Mbinga akimwelekeza mteja namna ya kutumia dawa.

Hivyo basi wadau wote wanakaribishwa kuwa sehemu ya jarida hili ambalo litahakikisha sauti zao zinasikika katika kueleza maendeleo ya mpango huu, huku likitoa nafasi ya kipekee ya kusimulia hadithi za watoa huduma wa DLDM (wamiliki na watoa dawa) na watumiaji wa DLDM, na kuitambua ipasavyo michango ya wadau wa maendeleo katika utekezaji mzima wa mpango.

Tahariri

Tuna furaha ya kuwaletea toleo la kwanza la Sauti ya DLDM, jarida linalolenga kuwapa sauti wadua katika utoaji wa habari za mpango wa DLDM. Jaridi hili litatolewa kila baada ya miezi mitatu. Katika toleo hili, tunapenda kutambua jitihada za Baraza la Famasi za kuongeza ufanisi katika usimamizi mzima wa mpango wa DLDM kupitia matumizi ya teknolojia ya kisasa ya mawasiliano. Pia tunapongeza uteuzi wa Bi. Elizabeth Shekalaghe kuwa Msajili wa Baraza la Famasi na kuangazia maoni yake kuhusu njia za kuendeleza utekelezaji wa mpango wa DLDM.

Katika toleo hili pia tunaangazia jitihada mbalimbali za kupunguza uhaba wa watoa dawa ambao ni tatizo kubwa nchini. Mafunzo ya hivi karibuni ya zaidi ya watoa dawa wa DLDM 120 katika Halmashauri ya Jiji la Arusha kwa michango ya fedha kutoka kwa watoa huduma wa DLDM, utoaji wa kozi ya mwaka mmoja ya watoa dawa inayoendeshwa na chuo cha afya cha St. Peter's kilichopo Dar es Salaam (St. Peter's College of Health Sciences); na mafunzo rejea kwa watoa dawa wa DLDM yaliyoendeshwa hivi karibuni mkoani Rukwa kwa msaada wa kifedha kukota shirika la PSI-Tanzania; vyote vinaonyesha nguvu ya ushirikiano

kati ya sekta binafsi na serikali katika kushughulikia mahitaji ya mpango wa DLDM.

Michango wa wadau wa maendeleo katika jitihada mbalimbali za kuendeleza mpango wa DLDM pia imeelezwa katika toleo hili. Kasi ya sasa ya vyama vya watoa huduma wa DLDM nchini na mafanikio ya Baraza la Famasi katika kuimarisha mfumo mzima wa usimamizi kwa kutumia teknolojia ya kisasa ya mawasiliano, yote hayangewezekana bila msaada mkubwa kutoka shirika la MSH kupitia mradi wake wa kuendeleza upatikanaji wa dawa katika sekta binafsi (SDSI project). Usambazaji wa mabango madogomadogo 4,300 ya kutambulisha maduka ya dawa muhimu kwa msaada wa PSI – Tanzania pia utasidia kuhimiza ununuzi wa dawa kutoka kwenye maduka yanayotambulika kisheria na kuongeza matumizi ya huduma za DLDM.

Katika kuendeleza mafanikio haya ya ushirikiano, tunapenda kuwakaribisha wadau wote wa DLDM kushirikiana nasi katika uandaji wa Sauti ya DLDM kwa kutoa uzoefu na maoni juu ya utekelezaji wa mpango wa DLDM. Uandaaji na usambazaji wa toleo hili umedhaminiwa na shirika la MSH kupitia mradi wa SDSI. Tunawashukuru sana kwa msaada wao.

wa DLDM nchini Tanzania, kiitwacho Ruvuma Drug Dispensing Outlets Association (RUDDOA).

Wenzao katika wilaya jirani ya Mbinga walifuatia mara baada ya muda mfupi kwa kuanzisha chama kiitwacho Mbinga Drug Dispensing Outlets Association

Inaendelea uk. 3



Hiki ndicho cheti chetu cha usajili:
Godfrey Sende, kitibu wa MBIDDOA

Majukumu na Faida

- Jukwaa la kutoa sauti ya pamoja katika kupigania haki na maslahi ya wanachama;
- Kuwawezesha wanachama kiuchumi kwa kuwashirikisha katika shughuli mbalimbali za kiuchumi;
- Kuboresha mahusiano ya kikazi baina ya watoa huduma wa DLDM (wamiliki na watoa dawa);
- Kuwa chombo maalum cha mazungumzo na majadiliano baina ya watoa huduma wa DLDM na mamlaka yanayosimamia shughuli za DLDM;
- Kuhamasisha ufuataji wa sheria na taratibu za DLDM kwa hiari;
- Kujenga na kuendeleza mahusiano na wadau wote wa DLDM kwa manufaa ya wote.

Vyama vya DLDM vyashika kasi

Tangu kuanzishwa kwa mpango wa DLDM, uanzishwaji wa vyama vya watoa huduma wa DLDM umepewa kipaumbele kama mkakati mmojawapo wa kuimarisha uendelevu wa mpango huu. Mnamo mwaka 2003 wakati wa majaribio ya mpango mkoani Ruvuma, wamiliki wa maduka ya dawa muhimu katika Manispaa ya Songea walianzisha chama cha kwanza cha watoa huduma

Vyama vya DLDM vyashika kasi



Sehemu ya wanachama wa CHAWAMAMU wakijivunia na kadi ya uanachama waliyopewa wakati wa uhamasishaji wa wanachama hoa wilayani Mbarali.

... Inaendelea kutoka uk. 2

(MBIDDOA) mnamo mwaka 2004. Kadri utekelezaji wa mpango wa DLDM ulivyoenea katika mikoa mingine, vyama zaidi vilianzishwa. Mpaka kuenea kwa mpango huo kitaifa mnamo Novemba 2013, vyama thelathini na nne vilikwisha anzishwa katika maeneo mbalimbali nchini.

Mkutano wa kitaifa wa wadau wa DLDM uliofanyika mkoani Tanga Septemba 2012 ulisisitiza umuhimu wa vyama hivyo. Mkutano ulipendekeza mikakati mbalimbali ya kuongeza kasi katika uanzishwaji wa vyama, kuboresha usimamizi na kuimarisha uendeleu wa vyama hivyo. Kwa kuyaitikia mapendekezo ya mkutano huo, shirika la Management Sciences for Health (MSH) kwa ushirikiano na Baraza la Famasi, limesaidia shughuli mbalimbali za kuimarisha vyama vya gDLDM nchini, nguvu zaidi zikielekezwa kwa vyama katika wilaya nne za majaribio za Mbinga, Mbarali, Kilombero na Bagamoyo.

Shughuli muhimu katika wilaya hizo za majaribio ni pamoja na uhamasishaji wa wamiliki wa maduka ya dawa muhimu

juu ya majukumu, faida na wajibu wa vyama; usambazaji wa vipeperushi na vitini maalum vya kuhamasisha umuhimu na usimamizi bora wa vyama; na ufuatiliaji wa karibu kujua maendeleo ya vyama na kutoa ushauri wa kitaalam kadri unavyo hitajika.

Juhudi hizi kwa kiasi kikubwa zimewapa motisha wanachama na kusababisha uongezeka kubwa wa wanachama hai katika baadhi ya maeneo. Makusanyo ya fedha kutokana na ada ya kila mwezi ya uanachama pia yameongezeka. Vyama vyote vinne katika wilaya za majaribio (yaani MBIDDOA cha Mbinga, CHAWAMAMU cha Mbarali, CHAWAMUKI cha Kilombero na BEDSA cha Bagamoyo) vimeandaa mipango kazi ya miaka mitatu na vinaanza kupiga hatua katika kujiendesha kwa njia rasmi.

Aidha, utoaji wa zana za uanachama kama vile rejesta, umeboresha utunzaji wa taarifa za wanachama na kurahisisha ufuatiliaji wa malipo ya ada za uanachama. Vyama vyote pia vimeonyesha nia ya kuhimiza ufuataji wa sheria za DLDM kwa kuweka katika mipango yao uhamasishaji wa ufuataji wa sharia kama ajenda ya kudumu

katika vikao vyao vote, na kuweka mifumo ya uongozi itakayowezesha wanachama kushiriki kikamilifu katika kujisimamia kisheria.

Katika ngazi ya taifa, shughuli zilizofanywa kuanzia Agosti 2013 ni pamoja na kuviainisha vyama vyote vya DLDM vilivyo kwisha undwa nchini; kuboresha vitini maalum vya kuhamasisha umuhimu na usimamizi bora wa vyama kwa kuviongezua taarifa muhimu za vyama vya ushirika na vyanzo vingine vya kujiwezesha kiuchumi; na kuandaa na kusambaza zana za uanachama kama vile kadi, cheti na rejesta, kwa baadhi ya vyama nchini.

Tarehe 23 Aprili 2014, mkutano mkubwa wa uhamasishaji wa kitaifa uliowakutanisha viongozi wa vyama 18 tofauti ulifanyika mkoani Morogoro. Vyama vilichaguliwa kutoka kanda zote saba za Tanzania Bara. Mkutano uliwapatia viongozi hao nafasi ya kipekee ya kubadilishana uzoefu na kujifunza kutoka kwa wenzao. Uwakilishi wa kanda zote katika mkutano huo ulizipatia shughuli za vyama vya DLDM sura ya kitaifa na kuchochea mazungumzo na mahusiano yanayoelekea uanzishwaji wa chama cha kitaifa.

Halmashauri ya Jiji la Arusha yakabiliana na uhaba wa watoa dawa wa DLDM

Uhaba wa watoa dawa katika maduka ya dawa muhimu ni changamoto kubwa katika maeneo mengi. Uhaba huo hutokana na sababu nyingi zikiwemo kuhama kwa watoa dawa waliofundishwa, kubadilisha fani, na ukosefu wa mpango endelevu katika halmashauri wa kutoa mafunzo kwa watoa dawa hao. Maduka ya dawa katika jiji la Arusha nayo yamekumbwa na tatizo hili, ikizingatiwa kwamba tangu kuanzishwa kwa mpango wa DLDM jijini humo mwaka 2011, hakuna mafunzo yoyote ya watoa dawa wa DLDM yaliyofanyika ili kukabiliana na ongezeko kubwa la uhitaji wa watoa dawa.

Kwa sababu hiyo, kati ya Aprili 14 na Mei 17, 2014, Halmashauri ya Jiji la Arusha kwa kushirikiana na wamiliki na watoa dawa wa DLDM, ilitoa mafunzo kwa watoa dawa kwa mara ya pili jijini humo. Mafunzo yalifanyika katika

Shule ya Kimataifa ya Arusha-Meru na yalikusishwa washiriki kutoka wilaya jirani ya Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Tofauti na mafunzo ya kwanza ambayo kwa kiasi kikubwa yalifadhiliwa na serikali, mafunzo ya pili yalifadhiliwa na washiriki kwa njia ya malipo ya ada.

Jumla ya watoa dawa 124 walishiriki kwenye kozi hiyo. Kati ya hao, 106 (85.5%) walikuwa wanawake. Wengi wa washiriki, 80 (64.5%) walikuwa wakazi wa Halmashauri ya Jiji la Arusha. Washiriki 44 (35.5%) walikutoka Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Kitaaluma, wengi wa washiriki (58%) walikuwa wauguzi wasaidizi, 26% walikuwa wauguzi waliosajiliwa, 11% wailikuwa maafisa wa afya na 5% walikuwa waganga wasaidizi.

Lengo la mafunzo hayo lilikuwa ni kuwapatia washiriki elimu ya msingi na ujuzi wa utoaji dawa. Kozi ilikuwa na

mada zifuatazo kulingana na mwongozo wa mafunzo ya DLDM: maadili, sheria, kanuni na taratibu za DLDM; mbinu bora za utoaji dawa; maelezo juu magonjwa mbalimbali, dalili na matibabu; utunzaji wa kumbukumbu; stadi za mawasiliano; afya ya uzazi na mtoto (hasa njia za uzazi wa mpango); na sehemu za mkakati wa kushughulikia magonjwa ya watoto kwa uiano (IMCI).

Mwishoni mwa mafunzo hayo, mtihani wa mwisho ulitolewa kwa washiriki wote 124, na 97 kati yao (78%) walifaulu mtihani huo. Washiriki waliofaulu walitunukiwa cheti cha utoaji dawa wa DLDM katika tafrija ya mahafali iliyoongozwa na mfamasia wa mkoa wa Arusha, Bw. Akwilina Maukion kwa niaba ya mganga mkuu wa mkoa. Tafrija hiyo ilishuhudiwa na Bw. Richard Silumbe, mratibu wa kitaifa wa mpango wa DLDM kwa niaba ya msajili wa Baraza la Famasi.



Sehemu ya watoa dawa wa DLDM wakitoa burudani wakati wa hafla ya mahafali baada ya mafunzo ya DLDM yaliyotolewa na Halmashauri ya Jiji la Arusha.

PSI-Tanzania yashirikiana na Baraza la Famasi kubadili muonekano wa maduka ya dawa muhimu



Mmiliki na mtoa dawa wa DLDM wakilifurahia bango jipya la DLDM lililotolewa na Baraza la Famasi.

Kati ya mwezi Aprili na Mei 2014, shirika la PSI-Tanzania ilishirikiana na Baraza la Famasi kusambaza mabango ya maduka ya dawa muhimu 4,300 nchi nzima. Zoezi hili lilikuwa sehemu ya lile la kitaifa la kubainisha maduka ya dawa muhimu yanayofanya kazi tangu mpango wa DLDM uenezwe nchi nzima.

Wakati wa zoezi hili, maduka yaliyothibitika kuendeshwa kwa viwango vinavyotakiwa yalipewa bango jipya yenye nembo ya mpango wa DLDM iliyochapwa kando ya ile ya Baraza la Famasi. Kuwekwa kwa nembo ya Baraza la Famasi kutasaidia kuwakumbusha watoa huduma wa DLDM (wamiliki na watoa dawa) pamoja na jamii kwa ujumla, wajibu wa Baraza la Famasi katika kudhibiti uendeshwaji wa maduka hayo.

Bango la DLDM limetumika tangu wakati wa majaribio ya mpango huu katika mkoa wa Ruvuma muongo mmoja uliopita, kama njia ya kuyapatia maduka ya dawa muhimu muonekano maalum. Bango hutolewa tu kwa maduka ambayo yametimiza masharti yote ya usajili (kwa mfano kuwa na mtoa dawa au watoa dawa waliofundishwa, hali ya njengo inayostahili utunzaji bora wa dawa na utoaji wa huduma, upatikanaji wa dawa bora kutoka kwenye vyanzo

vinavyokubalika kisheria n.k.) na yenye vyeti vya usajili.

Kazi yake muhimu ni kuwaelekeza wananchi mahali maduka ya dawa muhimu yalipo ndani ya jamii. Hivyo, utengenezaji na usambazaji wa mabango

4,300 utahamasisha ununuaji wa dawa kutoka kwenye vyanzo vinavyokubalika kisheria na kuongeza utumiaji wa huduma za DLDM - kwa haya yote msaada wa kifedha wa PSI-Tanzania hauna budi kutambuliwa na kupewa shukrani maalum.

Watoa dawa wa DLDM 358 mkoani Rukwa wapata mafunzo ya rejea

Mwezi Mei 2014, Baraza la Famasi kwa kushirikiana na halmashauri nne za wilaya za mkoa wa Rukwa (Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo na Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi) ilitoa mafunzo ya rejea kwa watoa dawa wa DLDM mkoani humo. Mafunzo yaliweka mkazo zaidi katika kuwaelimisha watoa dawa juu ya njia za uzazi wa mpango na mabadiliko katika miongozo ya tiba ya Malaria. Mafunzo yalitanguliwa na maelezo ya awali kwa jopo la wakfunzi ambalo lilikuwa na wafamasia kutoka halmashauri zote nne na wawezeshaji wa ngazi ya kitaifa. Mafunzo yalitolewa katika vituo viwili tofauti (Ribori na St. Bhakita) kwa wakati mmoja. Waliopewa mafunzo katika kituo cha Ribori walikuwa watoa dawa 258 kutoka Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri ya Wilaya ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Kalambo. Waliofundishwa katika kituo cha St. Bhakita walikuwa watoa dawa 100 kutoka Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi. Mafunzo hayo yalifadhiliwa na shirika la PSI-Tanzania kupitia Baraza la Famasi.

Kuna msemo usemao kwamba mazingira mapya huitaji mbinu mpya. Kutokana na kuongezeka kwa maduka ya dawa muhimu nchini kulikosababishwa na kuenezwa kwa mpango wa DLDM kitaifa, umuhimu wa kuwa na mfumo thabiti wa kudhibiti shughuli za maduka hayo unahitajika haraka.

Hadi Machi 2014, maduka ya dawa muhimu 5,757 yalikuwa yameanzishwa katika sehemu mbalimbali za Tanzania Bara na zaidi ya watoa dawa 18,980 walishapata mafunzo. Mafanikio haya yanamaanisha kuna mahitaji makubwa ya udhibiti kwa upande wa Baraza la Famasi na mamlaka nyingine husika, kuhakikisha maduka ya dawa yanafuata sheria na kutoa dawa bora na huduma zinazofaa kwa wananchi.

Ili kutimiza azma hii, Baraza la Famasi limeanzisha programu makini ya kuboresha mfumo wa udhibiti ambao utatoa kipaumbele kwa matumizi ya teknolojia ya kisasa ya mawasiliano katika usimamizi mzima wa mpango wa DLDM na shughuli zingine za udhibiti za baraza. Juhudi hizi zinaongozwa na mkakati wa kitaifa wa kutumia mawasiliano ya ki-ilektroniki kuendesha shughuli za serikali, ambao unalenga kuongeza utoaji wa huduma bora na kwa uharaka kwa wananchi na katika shughuli za kibiashara.

Kwa kiwango kikubwa, juhudi hizi zinasaidiwa na ukuaji haraka wa matumizi ya teknolojia ya habari na mawasiliano nchini, hasa ile ya simu za mkononi, na ongezeko la uhitaji wa kupata habari katika enzi hizi za kukua kwa matumizi ya teknolojia ya kidijitali.

Takwimu za karibuni za Mamlaka ya kudhibiti Mawasiliano Tanzania (TCRA) zinaonyesha kuwa idadi ya watumiaji wa simu za mkononi nchini imeongezeka kutoka 2.9 milioni mwaka 2005 na kufikia 27.4 milioni mwaka 2013, ikimaanisha karibu 60% ya watu wanaotumia simu za mkononi kwa sasa. Idadi ya watumiaji wa mtandao wa intaneti pia imeongezeka kutoka 3.5



Kifaa cha kuifadhia taarifa ndani ya chumba cha mawasiliano cha Baraza la Famasi.

milioni mwaka 2008 hadi 9.3 milioni mwaka 2013.

Uchambuzi wa hali halisi uliofanywa na shirika la MSH kwa kushirikiana na Baraza la Famasi mwaka 2012 ulionyesha kuwa wauzaji dawa wa jumla wote (100%) na asilimia tisini (90%) ya watoa huduma wa DLDM hutumia simu za mkononi katika shughuli zao za kibiashara.

Kutokana na taarifa hizi, Baraza la Famasi likisaidiwa na shirika la MSH kupitia mradi wake wa kuendeleza upatikanaji wa dawa kupitia sekta binafsi (SDSI project) limeanzisha mfumo maalumu wa utoaji na upokeaji taarifa kwa njia ya simu za mkononi na intaneti (integrated mobile information system) ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa mpango mzima wa DLDM na utekelezaji wa shughuli nyingine za udhibiti.

Mfumo huu una sehemu kubwa nne: (i) Sehemu ya kuhifadhi taarifa kwenye mtandao, (ii) Sehemu ya kutoa taarifa

juu ya viashiria maalum kwa njia ya simu za mkononi; (iii) Sehemu ya kufanya malipo kwa njia ya simu za mkononi na (iv) Sehemu ya kupeana taarifa.

Ili kuwezesha mfumo huu kufanya kazi ipasavyo, teknolojia za mawasiliano kwa njia ya simu za mkononi zenye uwezo wa kutumika kwenya simu za kawaida zimebuniwa kwa msaada wa kiufundi kutoka taasisi ya ITIDO, ambayo ni mkandarasi wa mradi wa SDSI unaosimamiwa na shirika la MSH.

Sehemu ya kuhifadhi taarifa kwenye mtandao itatoa taarifa za msingi juu ya DLDM na huduma za famasi nchini kote (kwa mfano hali ya usajili, sifa za wafanyakazi, hali ya huduma kutokana na ripoti za ukaguzi, hali ya majengo, malipo ya leseni, n.k.). Sehemu hii itaunganishwa kwenye mfumo maalumu wa Google unaoweza ufuatiliaji wa taarifa za maduka ya madawa kwa njia ya mtandao.

Utaratibu huu pia utawezesha wasimamizi wa mpango wa DLDM katika ngazi ya wilaya kupata na kutuma taarifa kupitia mfumo wa kielektroniki uliotengenezwa kwa ajili ya shughuli za udhibiti za kila mara (kwa mfano usajili, ufuatiliaji, ukaguzi, n.k.).

Sehemu ya kuhifadhi taarifa pia itaunganishwa na sehemu nyinginezo za mfumo maalum wa utoaji na upokeaji taarifa (sehemu ya kufanya malipo kwa njia ya simu za mkononi, sehemu ya kutoa taarifa juu ya viashiria maalum na sehemu ya kupeana taarifa) na kuratibiwa ili iweze kutoa ripoti kwa muhtasari katika nyakati mbalimbali. Taarifa na ripoti ambazo sio za siri zitapatikana katika tovuti ya Baraza la Famasi kwa ajili ya matumizi ya wananchi.

Sehemu ya kutoa taarifa juu ya viashiria maalum itawawezesha watoa

Inaendelea uk. 7



Watoa huduma wa DLDM wilayani Kibaha wakipewa mafunzo juu ya matumizi ya teknolojia ya mawasiliano ya kisasa katika shughuli za DLDM.

... Inaendelea kutoka uk. 6

dawa za DLDM na wahudumu wa famasi kuwasilisha ripoti juu ya viashiria vilivyochaguliwa kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu ya mkononi (kama vile upatikanaji wa bidhaa, utaratibu wa kutoa dawa, huduma kwa wateja n.k.). Kupitia njia hii, maofisa wa Baraza la Famasi katika ngazi zote na wasimamizi wa mpango wa DLDM wilayani wataweza kutuma ripoti za muhtasari za shughuli za usimamizi, ufuatiliaji na ukaguzi.

Taarifa kutoka kwa wadau wote zitatumwa kwa sehemu ya kuhifadhi taarifa ya Baraza la Famasi kwa muda unaotakiwa. Mfumo huu unategemewa kuongeza upatikanaji wa taarifa kwa wakati kwa ajili ya kupanga na kufanya maamuzi katika ngazi za sera na utekelezaji.

Sehemu ya kutoa taarifa itawawezesha watoa huduma wa DLDM na wafanyakazi wa famasi kuomba taarifa maalumu au ufafanuzi kutoka Baraza la Famasi na kutoa maoni au malalamiko juu ya masuala mbalimbali ya udhibiti. Hili litafanyika kwa njia ya ujumbe mfupi wa simu ya mkononi na barua pepe, ambao utatumwa kwa sehemu ya kuhifadhi taarifa na kuelekezwa kwa wafanyakazi wa Baraza la Famasi wanaohusika ili wachukue hatua inayofaa.

Kwaupande mwingine, Baraza la Famasi litatumia njia hii kutoa jumbe za tahadhari kwa simu za mkononi inapobidi kufanya hivyo (kwa mfano taarifa za ada, taarifa za usalama wa bidhaa na za kurudisha madawa yasiyofaa, n.k.). Sehemu hii inalenga kuleta uhusiano wa karibu kati ya Baraza la Famasi na watoa huduma za dawa katika ngazi zote, kukiwemo maduka ya dawa muhimu katika maeneo yasiyofikika kirahisi.

Sehemu ya malipo kwa njia ya simu za mkononi itawawezesha watoa huduma wa DLDM na wafanyakazi wa famasi kulipa ada za udhibiti kupitia huduma za fedha kwa njia ya simu za mkononi. Mfumo huu umeunganishwa kwa huduma za Vodacom M-Pesa katika awamu ya majaribio. Hata hivyo hii haizuii ushirikishwaji wa watoa huduma za fedha kwa njia ya simu wengine huko mbeleni.

Sehemu ya malipo ya fedha imeunganishwa na ile ya kuhifadhi taarifa ambayo moja kwa moja itaweka kumbukumbu za malipo na kumwarifu mlipaji mara moja, na pia Baraza la Famasi pale tatizo linapotokea. Uthibitisho wa malipo, taarifa za ukumbusho na za adhabu ya kuchelewesha malipo zitatumwa kwa ujumbe mfupi wa simu ya mkononi. Njia hii pia italiwezesha Baraza la

Famasi kutuma fedha kwa halmashauri za wilaya kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za udhibiti na kuongeza ufanisi katika ukusanyaji wa ada.

Maandalizi na uwekaji wa mfumo mzima wa utoaji na upokeaji taarifa kwa njia za simu ya mkononi na intaneti vilikamilika mwezi Machi 2014. Majaribio ya awali ya mfumo yaliyoanza Aprili 2014 yaliambatana na kutoa mafunzo kwa watoa dawa wa DLDM wa mkoa wa Pwani kuhusu jinsi ya kuutumia mfumo huu. Mafunzo yalikusishwa wilaya zote za mkoa wa Pwani (Kibaha, Bagamoyo, Kisarawe, Mkuranga, Rufiji na Mafia).

Mrejesho wa awali wa watumiaji unaonyesha kwamba watoa huduma wa DLDM kwa ujumla wanaridhika na mfumo huu. Athmini ya wataalamu wa nje kuhusu usalama wa mfumo itafanyika katika kipindi cha majaribio, na marekebisho muhimu yatafanyika ifikapo Augusti 2014 ili kuandaa mazingira ya kuueneza katika maeneo mengine nchini.

Mrejesho wa awali wa watumiaji unaonyesha kwamba watoa huduma wa DLDM kwa ujumla wanaridhika na mfumo huu.

Kundi la kwanza la wanafunzi wa kozi ya mwaka mmoja ya utoaji dawa wafanya mitihani ya kuetimu

Mwezi Mei 2014, kundi la kwanza la wanafunzi wa kozi mpya ya mwaka mmoja ya utoaji dawa (ngazi ya cheti) lilifanya mitihani ya kuetimu katika Chuo cha Afya cha St. Peter's (St. Peter's College of Health sciences) kilichopo Dar es Salaam. Chuo hicho kimekuwa cha kwanza nchini kusajiliwa na Baraza la Famasi kutoa kozi hiyo. Wanafunzi 15 waliandikishwa katika darasa la kwanza Aprili 2013, kati yao 12 walimaliza kozi na kufanya mitihani ya kuetimu.

Kozi hii imeanzishwa kwa lengo la kupunguza upungufu mkubwa wa watoa dawa katika ngazi ya chini. Ingawa mafunzo mafupi kwa watoa dawa wa DLDM kupitia halmashauri za wilaya yamesaidia kupunguza mapengo kwa kiasi fulani, ukosefu wa mafunzo ya mara kwa mara umekuwa chanzo kikubwa cha upungufu wa watoa dawa nchi nzima.

Aidha, kwa vile muda wa kozi ya watoa dawa wa DLDM ni mfupi (siku 35), na ukizingatiwa kwamba haijasajiliwa na Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) chini ya mfumo wa vyeti vya ufundi vya kitaifa, haiwawezeshi watoa dawa waliopata mafunzo hayo kuendelea moja kwa moja na masomo katika ngazi ifuatayo ya mafunzo ya kitaaluma ya famasi (kozi ya mfasia msaidizi).

Kikwazo kingine cha kozi ya muda mfupi ya watoa dawa wa DLDM ni kwamba kundi la walengwa muhimu (manesi wasaidizi) ni aina ya wafanyakazi ambao wanafutwa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, hivyo kuwapata waombaji wa kozi hii wenye sifa zinazohitajika ni jambo ambalo linazidi kuwa gumu.

Kwa sababu hii, Baraza la Famasi lilianzisha kozi ya watoa dawa kwa ngazi ya cheti kama hatua ya muda mrefu ya kupunguza tatizo la watoa dawa waliopata mafunzo katika maduka binafsi yenye kuuza dawa kwa rejareja.



Wanafunzi wa chuo cha afya cha St. Peter's Dar es Salaam wakifanya mitihani wa kuetimu kozi ya mwaka mmoja ya utoaji dawa iliyoanzishwa na Baraza la Famasi.

Uandaaji wa mtaala ulianza kikamilifu mwaka 2009 na ulipitia katika mchakato wa marekebisho uliopelekea kozi hiyo kusajiliwa na NACTE kama mpango wa mafunzo wa cheti cha kitaifa cha ufundi ngazi ya 4. NACTE pia ilitoa mamlaka kwa Baraza la Famasi kudhibiti ubora wa mafunzo, kutunga na kutoa mitihani na kutoa vyeti kwa wanafunzi waliofaulu.

Muda wa kozi hiyo ni mwaka mmoja. Kozi ina moduli 12 zinazotolewa katika miula miwili (moduli 6 kila muhula), ikifuatiwa na mwezi mmoja wa mafunzo kwa vitendo. Mtoa dawa yeyote wa DLDM aliyemaliza kozi fupi ya siku 35 ya watoa dawa DLDM na kufaulu mitihani ya mwisho, au mhitimu wa kidato cha nne aliyefaulu (daraja D) katika masomo ya biolojia na kemia, anastahili kujiunga na kozi hii.

Baada ya kumaliza mafunzo, wanafunzi waliofaulu hupokea cheti cha NTA ngazi ya 4 ya utoaji dawa, na wanaweza kuendelea na ngazi ya 5 ya NTA (cheti cha famasi) ambayo ni kozi ya miaka miwili. Kwa njia hiyo, kozi hii ya mwaka mmoja ya utoaji dawa hufungulia njia waliofaulu kujiendeleza kimasomo katika taaluma ya famasi.

Kozi hii inaweza kutolewa na chuo chochote cha elimu cha kati kilichoidhinishwa na chenye uwezo wa kiufundi kutoa kozi hiyo kwa ufanisi unaotakiwa. Mbali na chuo cha afya cha St. Peter's, vyuo vingine vitano vimepewa vibali na Baraza la Famasi kutoa kozi hiyo. Vyuo hivyo ni pamoja na Royal Pharmaceutical Training Institute, Dar es Salaam College of Health Sciences, City College of Health Sciences and Kam College of Health Sciences and Paradigm Pharmacy College. Vyuo hivyo vyote viko jijini Dar es Salaam.

Utoaji wa kozi hiyo katika taasisi hizi utahakikisha uzalishaji wa watoa dawa na kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa watoa huduma hawa katika maduka ya dawa ya rejareja yanayomilikiwa na watu binafsi.

Utoaji wa kozi hii katika taasisi za mafunzo utahakikisha uzalishaji wa watoa dawa na kusaidia kupunguza tatizo la uhaba wa watoa huduma hawa katika sekta binafsi.



Msajili wa Baraza la Famasi azungumzia dira ya mpango wa DLDM

Swali 1: Ikiwa ni chini ya miezi miwili tangu uteuliwe kuwa Msajili wa Baraza la Famasi, unajisikiaje kupewa jukumu hili jipya na kubwa?

Nimejawa na shukrani kwa fursa hii ya kuitumikia nchi yetu katika wadhifa huu. Nafahamu kuwa ni jukumu zito ila naamini kwamba kwa kufanya kazi kwa ushirikiano na wenzangu kama timu tutaweza kuutimiza wajibu wetu.

Swali 2: Kabla ya kuhamishwa kwa mpango wa DLDM kutoka Mamlaka ya Chakula na Dawa Tanzania (TFDA) kwenda kwa Baraza la Famasi, ulikuwa mratibu wa kitaifa wa mpango huu chini ya TFDA. Je, utakuwa na mchango gani katika utekelezaji wa mpango huu kama Msajili wa Baraza la Famasi?

Kama msajili, jukumu langu ni kusimamia shughuli zote za Baraza la Famasi. Usimamizi wa mpango wa DLDM ni mojawapo ya kazi muhimu za Baraza.

Swali 3: Mpango wa DLDM umepitia mchakato mpana wa utekelezaji kuanzia majaribio mkoani Ruvuma muongo mmoja uliopita hadi upanuzi wa kimkoa na kitaifa. Je, mpango



Bi. Elizabeth Shekalaghe

huu utakuwa na shughuli zipi katika awamu inayofuatia baada ya kuupanua kitaifa?

Tangu kuanzishwa kwake, mpango wa DLDM umelenga kuongeza upatikanaji wa dawa bora na huduma zinazofaa kwenye maeneo ya vijijini na pembezoni mwa miji ambapo huduma za dawa hazitoshi au hazipo kabisa. Tunapoelekea, tunataka kuweka msisistizo zaidi katika kuendeleza na kuimarisha mafanikio yalipatikana mpaka sasa kwa kuweka kipaumbele katika ubora wa huduma na matumizi yenye tija ya huduma za DLDM.

Kwa hiyo, tunadhamiria kufanya yafuatayo: (i) kuongeza idadi ya watoa dawa wenye ujuzi unaofaa kwa kuweka mifumo ya kitaasisi ya kutoa mafunzo endelevu kwa watoa huduma hao kupitia taasisi za umma na za binafsi; (ii) kushirikiana kwa karibu zaidi na halmashauri za wilaya na kuziwezesha kuwa mstari wa mbele katika kusimamia sheria, kanuni na viwango vilivyowekwa kwa ajili ya shughuli za DLDM; (iii) kuhamasisha watoa huduma wa DLDM kujidhibiti na kujisimamia wenyewe kupitia vyama vyao; (iv) Kuongeza ufanisi katika mfumo mzima wa udhibiti kwa kutumia ipasavyo teknolojia ya kisasa ya mawasiliano; na (v) kufanya tathmini za mara kwa mara kufuatilia maendeleo ya mpango, kuainisha maeneo yanayohitaji kuboreshwa na kusanya taarifa muhimu za kusidia uandaaji wa sera na mipango ya utekelezaji kwa kutegemea ushahidi wa kitafti. Pia tunapanga kutumia uzoefu uliopatikana katika mikoa mbalimbali kuhamasisha matumizi ya DLDM kama njia bora ya kufikisha baadhi ya huduma za afya ya jamii kwa wananchi.

Swali 4: Je, ni mafanikio gani ya mpango wa DLDM ambayo yamepatikana mpaka sasa, na Baraza lina mpango gani wa kuyaendeleza?

Tunapoelekea tunataka kuweka msisistizo zaidi katika kuendeleza na kuimarisha mafanikio yalipatikana mpaka sasa kwa kuweka kipaumbele katika ubora wa huduma na matumizi yenye tija ya huduma za DLDM.

Ushahidi kutoka tafti mbalimbali umeonyesha kuwa mpango wa DLDM unachangia kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa dawa muhimu, hasa katika maeneo ya vijijini na yaliyo pembezoni mwa miji na kuboresha utoaji wa dawa. Pia umesaidia kuboresha hali ya kuhifadhi dawa na mazingira ya utoaji huduma kwa ujumla.

Kama nilivyosema awali, tumebainisha maeneo maalumu ambako tunataka kuelekeza nguvu zetu ili kuendeleza na kuimarisha mafanikio ya mpango huu. Miongoni mwa mikakati tunayopanga kuitekeleza ni pamoja na: kuimarisha uratibu wa kazi katika ngazi zote (za kanda, mikoani, halmashauri na jamii); kuimarisha ushirikiano wa kitaasisi na wadau mbalimbali wakiwemo TFDA, halmashauri, programu za kitaifa za afya, wahisani na sekta binafsi; na kuongeza juhudi katika utafutaji wa rasilimali fedha ili kufanikisha utekeleza wa shughuli zilizopangwa.

Swali la 5: Ni changamoto zipi kubwa zimejitokeza mpaka sasa katika utekelezaji wa mpango wa DLDM, na Baraza limejipangaje kukabiliana nazo?

Baadhi ya changamoto kubwa ambazo zimejitokeza mpaka sasa ni pamoja na uhaba wa watoa dawa waliofundishwa licha ya jitihada za mpango kutoa mafuanzo kwa watoa dawa wa DLDM; usimamizi usioridhisha wa sheria, kanuni na viwango vya DLDM kutokana

Inaendelea uk. 10

... Inaendelea kutoka uk. 9



na shughuli za ukaguzi na ufuatiliaji kutopewa kipaumbele na baadhi ya halmashauri; na ugumu wa utekelezaji wa mpango huu katika miji mikubwa, hali ambayo imesababisha kuwepo kwa maduka ya dawa baridi pamoja na ya dawa muhimu katika miji husika.

Katika kukabiliwa na upungufu wa watoa dawa wenye ujuzi, Baraza la Famasi limeanzisha kozi ya mwaka mmoja ya cheti kwa ajili ya watoa dawa katika vyuo vya elimu vya kati, na limechukua hatua muhimu ya kuingiza rasmi kozi fupi ya watoa dawa wa DLDM katika mfumo wa kitaasisi wa vituo vya serikali vya mafunzo ya afya vya kikanda - wakati huohuo Baraza limeendelea kuhamasisha ushirikiano kati ya watoa huduma wa DLDM na halmashauri katika kuandaa mafunzo ya watoa dawa wa DLDM kadri yanavyohitajika.

Kuhusu usimamizi wa sheria, kanuni na viwango vya DLDM, Baraza la Famasi limeanzisha ofisi za kanda zitakazofanya kazi pamoja na mikoa kutoa msaada wa kitaalam kwa

halmashauri ili kuhakikisha shughuli za udhibiti zinapewa kipaumbele.

Hata hivyo, utekelezaji wa mpango katika miji mikubwa bado ni changamoto ambayo inahitaji majadiliano zaidi katika ngazi ya sera na ushirikishwaji wa kutosha wa wadau husika katika kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa baadhi ya vikwazo vilivyopo sasa.

Swali la 6: Uteuzi wako umepokelewa vizuri na wadau wengi katika sekta ya famasi nchini ambao wanakutegemea kuleta uongozi utakaoliwezesha Baraza la Famasi kumudu ipasavyo majukumu yake ya udhibiti yaliyoongezeka yakiwemo usimamizi wa mpango wa DLDM. Una mpango gani wa kutimiza jukumu hili?

Awali ya yote, napenda kuwashukuru wadau wote kwa kuwa na imani na mimi katika wadhifa huu. Ni kweli kwamba wigo wa mamlaka ya Baraza la Famasi umeongezeka kwa kiasi kikubwa kufuatia kupitishwa kwa Sheria ya Famasi ya mwaka 2011, na hii ni changamoto kubwa kutokana na

uwezo mdogo wa kitaasisi wa Baraza uliopo sasa.

Kipaumbele cha kwanza katika ajenda yangu ni kuimarisha uwezo wa ndani wa Baraza, hasa kwa upande wa rasilimali watu na vitendeakazi muhimu ili Baraza liweze kufanya kazi ipasavyo. Ningependa pia kuweka juhudi zaidi katika kukuza na kuimarisha ushirikiano na wadau mbalimbali ili kuweza kuongeza upatikana wa rasilimali watu, fedha na vifaa muhimu kwa ajili ya shughuli za udhibiti. Naamini ushirikiano wa karibu haswa kati ya Baraza la Famasi na TFDA utakuwa na manufaa makubwa kwa sekta ya dawa nchini. Ningependa kuwa mstari wa mbele kuendeleza ushirikiano huo.

Swali la 7: Ni ujumbe gani ungependa kuwapa wadau wa DLDM wanaosoma jarida hili?

Napenda kuwajulisha wote kwamba Baraza la Famasi linathamini kwa dhati mchango wao na liko tayari kushirikiana na kila mmoja wao kufankikisha lengo kuu la mpango wa DLDM.

